# FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2026 KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KAGERA RIVER WILAYA YA KARAGWE MKOA WA KAGERA S. L. P. 452, KARAGWE

**SIMU: Mkuu wa shule 0756317322 Makamu: 0753157662 Mtaaluma 0744663913 Nidhamu 0783680425**
**Email: kagerarivergirls2024@gmail.com**

Jina kamili la mwanafunzi: ________________________________________________

PREM NA. ______________________ kutoka shule ya msingi: ______________________

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha **kwanza,** katika shule hii mwaka 2026. **Unapaswa kuripoti shuleni siku ya jumatatu tarehe 05/01/2026,** kwahiyo maandalizi yafanyike kwa wakati. Ikiwa kuna kipengele katika fomu hii hakieleweki mzazi awasiliane na uongozi wa shule kwa namba zilizopo hapo juu.

## MAELEKEZO NAMNA YA KUFIKA SHULENI.

Uliza kama kuna magari yanayoelekea karagwe (Mkoa wa kagera) kutoka unakotokea kama yapo nenda hadi Kayanga. Kama hayapo, panda ya bukoba. Kama utatumia usafiri wa anga au maji, ukifika bukoba mjini, tafuta magari yanayoelekea Karagwe na ushuke stendi ya Kayanga (nauli ni sh. 5,000 safari ya masaa mawili). Ukifika stendi ya Kayanga tafuta magari yanayoenda Rwambaizi (nauli ni sh 4,000 safari ya dakika 40). Ukifika Rwambaizi taja jina la shule Kagera river sekondari utapelekwa shuleni kwa pikipiki (nauli ni sh. 2000 safari ya dakika tano).

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 1. SARE YA SHULE

- **Mwanafunzi anatakiwa kuja na mahitaji yafuatayo:-**

(i) Mashati meupe mawili yenye mikono mifupi inayoishia kwenye kiwiko cha mikono na yasiyobana mwili. (Mashati ya mikono mirefu kwa wenye mahitaji maalumu(Wenye Ualbino)

(ii) Nguo za kuvaa ndani ya shati ambazo ni sidiria au vesti ziwe za rangi nyeupe haturuhusu uvaaji wa nguo zenye rangi tofauti na nyeupe ndani ya shati la shule.

(iii) Sketi mbili (2) za rangi ya kijani jeshi mshono wa (rinda mojakubwa mbele na nyuma na marinda manne kulia na kushoto maarufu kama mishono ya masista wa RC).

(iv) Viatu vyeusi vya ngozi Jozi 2 vyenye visigino vifupi. Haturuhusu viatu vingine vyenye urembo wa aina yoyote.

(v) Buti nyeusi pea moja kwa ajili ya kuvaa wakati wa mvua kubwa na wakati wa kazi za nje.

(vi) Jozi tano za soksi nyeupe zisizo na mistari ya aina yoyote (free size/stocking) zinazofika magotini.

(vii) Wanafunzi wa Kiislamu waje na **Juba** nyeupe mbili, juba za maroon mbili na za rangi ya kijivu mbili ndefu zinazofunika kifua, zisizo na urembo wa aina yoyote.

(viii) Tai ya rangi ya kijani jeshi kilichokolea yenye nembo ya shule.

(ix) Masweta mawili ya rangi ya kijani jeshi kilichokolea yenye nembo ya shule.

(x) Tisheti ya rangi ya kijivu yenye kola na nembo ya shule.

(xi) Shamba dress (Gauni mbili ndefu za rangi ya maroon (damu ya mzee) mshono wa solo kitambaa kizito, kwa ajili ya kushindia na kazi za nje)

(xii) Traki suti nzito ya rangi ya kijivu (yaani suruali, tisheti na sweta)

(xiii) Koti kubwa na zito jeusi kwa ajili ya kujikinga na baridi hasa wakati wa usiku.

(xiv) **Kwa ajili ya michezo:** Tisheti nyekundu isiokuwa na kola, Sketi fupi nyekundu isiyovuka magoti, skini ndefu nyeusi, raba nyeupe na jezi ya njano iliyokamilika (yaani bukta na tisheti).

***ZINGATIA:***

a. ***Sare zifuatazo zinapatikana karibu na shule kwa bei zifuatazo kwa atakayehitaji (Sketi moja 25,000, Shamba dress moja 20000, Tai 5000, Tisheti ya kijivu (sio ya truck) 16000, Sweta 17000 na truck suti 25,000***
b. ***Sare zote ziwekewe alama ya utambuzi ili kudhibiti wizi (weka alama itayokusaidia kuzitambua nguo zako ila isionekane wazi na kuharibu mwonekano wa nguo)***

## 2. MAHITAJI MENGINE MUHIMU YA MWANAFUNZI

a) Madaftari 12 counter Books (Quire 3), kalamu za risasi na za wino, mkebe wa vifaa vya Hisabati **(Mathematical set) na *Elemenatry learners Dictionary* na Kadi ya Bima ya afya.**

b) **Nakala moja ya cheti cha kuzaliwa cha mwanafunzi.**

c) Godoro size 2.5’X6’, Blanketi1, Chandarua nyeupe ya duara, shuka 3 za blue bahari, foronya ya blue bahari moja na mto mmoja

### 3. Mahitaji mengine ya kibinadamu:

(i) Tranka (sanduku) kubwa1 kwa ajili ya usalama wa vitu vyake na kufuli imara kwa ajili ya kufungia tranka hilo.

(ii) Vyombo vya chakula (sahani ya bati nzito, kijiko na kikombe cha bati).

(iii) Picha 4 passport size akiwa amevaa shati la shule(jeupe) na ziwe na “background”(kivuli) ya bluu nyuma.

(iv) Taulo, Vitenge au Kanga doti moja atajifunga wakati wa kwenda kuoga.

(v) Viatu vya wazi (open shoes) kwa ajili ya kushindia.
(vi) Ream mbili za karatasi (A4) aina ya A one au double B
(vii) Mafaili mawili makubwa (Box files)
(viii) Kotama moja
(ix) Jembe moja na mpini wake
(x) Fyekeo (kwanja)
(xi) Mifagio (chelewa moja, soft broom moja na squizer moja)
(xii) Ndoo mbili (za lita 20 kila moja)
(xiii) Beseni moja kwa ajili ya kufulia
(xiv) Kidumu cha lita tano kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa.
(xv) Sabuni miche minne (4) gramu 800 kila moja, Mafuta ya kujipaka kopo kubwa, Toilet paper tano kubwa, Dawa ya meno, Mswaki, Dawa ya viatu na Brashi yake, Kata kucha isiyo na kisu. (Vitu vyenye ncha kali haviruhusiwi)
(xvi) Nguo za ndani za kutosha, gagulo(underskirt).
(xvii) Tochi inayotumia mwanga wa jua(solar) au betri. (Tochi za kuchaji kwa umeme haziruhusiwi)

**KUMBUKA:**

***Simu haziruhusiwi shuleni, hivyo kwa namna yoyote ile mwanafunzi asije na simu shuleni wala kifaa chochote kinachohusiana na simu kama vile chaja, seli, laini, earphone.**

*** Mwanafunzi analazimika kuvaa sare za shule wakati wote awapo shuleni, hivyo asije na nguo za nyumbani bali aje akiwa amevaa shamba dress au tracksuit.**

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Tekinolojia na Ufundi, yenye dhamana ya Elimu chini ya ofisi ya Rais– TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi hapa chini na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

(a) Heshima kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) **Mwnafunzi akimwona mtu mzima ni sharti asimame na kumsalimia na endapo ana mzigo ampokee.**
(c) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(d) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).
(e) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(f) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(g) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(h) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(i) Mwanafunzi atalazimika kuzingatia ratiba ya shule wakati wote awapo shuleni.

(j) Kutunza maliza shule na kuzilinda ni jambo la lazima.

(k) Mwanafunzi analazimika kuhudhuria vipindi vyote vya dini kwa mujibu wa ratiba ya shule.

**MUHIMU :** Ni marufuku kuvaa kanda mbili wakati wa chakula katika Bwalo au mazingira yoyote ndani na nje ya shule, isipokuwa bafuni wakati wa kuoga na bwenini.

- Wageni wa mwanafunzi wanaotambulika shuleni ni wale walioandikishwa kwenye faili la mwanafunzi na wanaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi mara moja tu kwa muhula yaani (mara 2 kwa mwaka).
- Likizo zote mwanafunzi atakapolazimika kwenda likizo ni sharti arudi nyumbani kwa wazazi/walezi wake, haruhusiwi kwenda kwa ndugu (Ubalozini) kipindi cha likizo fupi wala ndefu.
- Mzazi unatakiwa kuandaa pesa ya nauli ya kuja likizo fupi (kipindi cha Pasaka na Septemba)na likizo ndefu, mwezi Juni na Desemba na kuituma shuleni pindi tu itakapohitajika (utajulishwa ni lini utume nauli).
- Mwanafunzi harusiwi kuwa na urembo wa aina yoyote kama vile hereni, bangili, mkufu na pete za aina yoyote ile shuleni.
- Shuleni haturuhusu nywele ndefu hivyo mwanafunzi anatakiwa kuja na nywele fupi na asinyoe mtindo wa aina yoyote ile.
- Mwanafunzi awapo shule atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa, ni marufuku mwanafunzi kulala au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa, akishindwa kuzingatia atafukuzwa shule.

**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:**

1. Wizi.
2. Uasherati.
3. Usagaji.
4. Ulevi na matumizi ya Madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli na kadhalika.
5. Kupigana au kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau Bendera ya Taifa.
8. Kuwa mjamzito/kupata mimba.
9. Kuolewa ama kuwekwa kimada.
10. Kutoa mimba.
11. Kugoma, kuchochea, kuongoza, au kushiriki migomo na kuvuruga amani na usalama wa shule na usalama wa watu wengine.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Kutoroka shuleni mchana au usiku.
14. Kuwa na simu ya mkononi shuleni au kumiliki kifaa chochote kinachohusiana na simu(line, earphone, charger n.k).
15. Kuhama bweni alipopangiwa na kulala bweni jingine bila ruhusa.
16. Kuhamisha taa ya umeme(bulb) kutoka eneo moja kwenda kupachika eneo jingine.
17. Kubadili dini awapo shuleni tofauti na aliyoandika wakati wa kuripoti shuleni.

**MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKABIDHIWA SHULENI NA MWANAFUNZI PINDI TU ANAPORIPOTI.**

(i) Fomu ya kupimwa afya yake (Medical Examination form) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapo ripoti shuleni.

(ii) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

(iv) Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**Muhimu:- Tafadhali njoo na fomu hii ikiwa imejazwa kikamilifu.**

**MWL. FELISTER M. FRANCIS**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YA
WASICHANA-KAGERA RIVER
S.L.P ___ KARAGWE

**MKUU WA SHULE**

**FORM NO.1**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA PRESIDENTS' OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a medical Officer in respect of all Form I.

1. Pupil's full Name: ______________________________________________________
2. Age/Years ___________ Sex___________
3. Blood found (red and White)________________________________________________
4. Stool examination__________________________________________________________
5. Venereal Diseases test: ___________________________________________________
6. T.B. test:_________________________________________________________________
7. Eye test: _________________________________________________________________
8. Ears: _____________________________________________________________________
9. Chest: ____________________________________________________________________
10. Spleen: ___________________________________________________________________
11. Abdomen: __________________________________________________________________
12. Urine for Pregnant: _______________________________________________________

ADDITIONAL INFORMATION (If any) e.g. Physical defects, impairment (s) e.g. arm, leg etc. Infection chronic or family disease etc.

_____________________________________________________________________________________

_____________________________________________________________________________________

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature: ________________

Designation ________________________________________

Station: ___________________________________________

Date:_______________________

Official Stamp.

**FORM NO.2**

## SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KAGERA RIVER

### TAARIFA ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la mwanafunzi: ____________________________________________________
   Alizaliwa tarehe ________________
   Katika wilaya ya __________________________
   Dini yake ni ________________________ katika dhehebu la ________________________

2. Anwani ya mzazi/mlezi:
   Kijiji/Mtaa ___________________
   Kata ___________________
   Wilaya ___________________
   Mkoa ________________________

3. Kazi ya baba/mlezi ____________________________________________________

4. Kazi ya mama______________________________________________________

5. Majina ya wazazi au walezi wanaohusika na malezi ya huyu mwanafunzi (matatu tu), anuani zao kamili na Namba zao za Simu.Weka picha ya ndugu husika kwenye kiboksi kilichopo mbele ya jina lake.

(a) Jina la ndugu wa kwanza kutafutwa kwa taarifa yoyote: ___________________________________
Uhusiano na Mwanafunzi _____________________________
Simu__________________________
Ambatanisha picha yake kwenye boxi la kwanza

(b) Jina la ndugu wa pili: _________________________________________________
Uhusiano na Mwanafunzi____________________________
Simu_____________________________
Ambatanisha picha yake kwenye boxi la pili

(c) Jina la ndugu wa tatu: _____________________________________________
Uhusiano na Mwanafunzi____________________________________________________
Simu__________________________________
Ambatanisha picha yake kwenye boxi la tatu

……………………………………

**SAINI YA MWANAFUNZI (Isiwe ya kukoroga)**

TAREHE:……………………..

**FORMNO.3**
**MKATABA/AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi_____________________________________________ **(jina kamili la Mwanafunzi)** ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii. Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote. Naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote.

Jina la Mwanafunzi ______________________________________________________

Saini ya mwanafunzi (sio ya kukoroga) ______________________________

Tarehe______________________

**Shahidi (Mzazi au mlezi wake)**

Jina kamili ________________________________________________

Saini ________________________ Tarehe__________________________

**FORM NO.4**

**A: AHADI YA MZAZI:**

Mimi _______________________________________ (jina kamili la mzazi au mlezi) ambaye ni mzazi/mlezi wa ___________________________________ Kidato cha kwanza 2026, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vyema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii. Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo. Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

Saini ya Mzazi/Mlezi __________________

Simu:___________________________

Tarehe:_______________________

## FOMU NA 05
## MUONEKANO WA BAADHI YA SARE ZA WANAFUNZI











